
**Fisi maji koo madoa ( H. maculicollis) - Wanatishiwa kutoweka (IUCN Red list)**





Fisi maji koo-madoa ana takribani uzito wa 3-6kg, ni wa pili kwa udogo kati ya spishi zote 13 za fisi-maji duniani. Anafahamika kwa urefu na wembamba wa umbo la mwili (.62-<1m kwa wale wakubwa) mkia wa kuburuza, miguu mifupi, manyoya mengi na meusi(weusi ambao haujakolea) madoa meupe kwenye midomo, koo,au tumboni na vidole vya miguu vimeunganishwa na ngozi nyembamba inayomwezesha kuogelea vizuri ndani ya maji.

Chakula chake zaidi ni samaki, kaa lakini wanaweza kula viumbe waishio majini kama vyura/au wadudu jamii ya panzi kama wanapatikana kwa wingi.

Fisi maji kihistoria walikuwepo kwa wingi katika maziwa mito/vijito yenye maji safi na meupe kote barani Afrika. Mara nyingi huonekana mmoja au jike na watoto. Hata hivyo, madume, watoto wanaobalehe and pengine majike bila ya watoto wamewahi kuonekana katika makundi ya hadi fisi-maji 20. Mara nyingi zaidi fisi-maji <10.

Wanawinda kwa kutegemea zaidi macho hivyo wanahitaji maji safi na meupe ili kufanikisha kukamata windo lake.

Kujipatia joto la mwili wanapoteza muda mwingi zaidi katika kusugua manyoya yake kwenye magogo, nyasi au miamba ya mawe. Hii huvuruga manyoya ya ngozi yake na hewa kupenya nje na ndani ya ngozi iliyofumikwa na manyoya.






Mguu wa mbele kushoto na nyayo yake. 40-45 mm upana.
Unyayo wa dume ni mkubwa kuliko wa jike.

Kinyesi-Kibichi (chini) cha zamani juu (Kulia)







Kinyesi mithili ya mrija 11 – 21 mm mduara kinaweza pia kuonekana



Choo, mahali ambapo kinyesi hurundikwa inaweza kuchukua eneo mita kadha

Usichanganye nyayo au kinyesi cha fisi-maji  na kile cha Nguchiro-maji (Chini)





Nyayo za Nguchiro +/-30mm upana



Kinyesi cha Nguchirro-maji-
Mabaki ya kaa, nywele za wanyama wadogowadogo, vyura, wadudu,  ndege,  kwa makadirio 15-22mm mduara.



**Nguchiro-maji**
2 – 5.4kg
Manyoya marefu na yamesimama,
mkia una manyoya mengi.
Hujishughulisha zaidi usiku na peke yake.
Huishi nchi kavu kandokando ya mito

Taarifa watakapoonekana. Lini wameonekana, wapi, wangapi na taarifa zingine zaidi zinaweza kutumwa kwa africanotternetwork@gmail.com. Maswali pia yanakaribishwa!